**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE UZINDUZI WA MTAMBO WA KUSAFISHA DHAHABU**
**MWANZA, TAREHE 13 JUNI, 2021**

*Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini;*

*Waheshimiwa Mawaziri wengine mliopo;*

*Naibu Katibu Mkuu wa CCM;*

*Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel,*
*Mkuu wa Mkoa wa Mwanza na Wakuu wa Mikoa Jirani;*

*Waheshimiwa Wabunge mliopo;*

*Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini pamoja na Makatibu Wakuu wengine mliopo;*

*Meja Jenerali Mstaafu Michael Isamuyo,*
*Mwenyekiti wa Bodi ya STAMICO;*

*Bw. Anand Mohan, Mtendaji Mkuu wa Mwanza Precious Metal Refinery (MPMR);*

*Viongozi na Watumishi wa STAMICO na MPMR;*

*Viongozi wa Dini na Vyama vya Siasa mliopo;*

*Ndugu Wadau wa Sekta ya Madini mliopo;*

*Wageni Waalikwa, Wanahabari, Mabibi na Mabwana;*

**Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**SALAMU**

- Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia neema ya uhai na kutuweza kutukutana hapa tukiwa wenye afya njema. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Madini pamoja na Uongozi wa

Kampuni ya *Mwanza Precious Metals Refinery Limited* (MPMR) kwa kunikaribisha kwenye Uzinduzi wa Mtambo wa Kusafisha Dhahabu (*Refinery*) hapa Mwanza. Ahsanteni sana.

- Kwa namna ya pekee, nawashukuru na kuwapogeza Viongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa mapokezi yenu mazuri. Nawashukuru pia wananchi ambao mmejitokeza kwenye Hafla. Leo ni Jumapili; ni siku ya mapumziko na shughuli ya ibada; lakini mmeweza kijitokeza kwa wingi kunipokea. Ahsanteni sana. Hii inadhihiri kuwa mnatambua umuhimu wa Mtambo huu kwa maendeleo na ustawi wa Mkoa wenu wa Mwanza na nchi yetu kwa ujumla.

**Waheshimiwa Viongozi;**
**Wageni Waalikwa Mabibi na Mabwana;**

- Hivi punde nimezindua Mtambo wa Kusafisha Dhahabu. Kama tulivyosikia, Mtambo pamoja na ujenzi wa Kiwanda na Ofisi mbili vimegharimu **shilingi bilioni 12.2**. Tumeambiwa pia kuwa Mtambo huu ni mkubwa na wa kisasa, ambapo uwezo wake ni kusafisha **kilo 480** za dhahabu; lakini zinaweza kuongezeka hadi kufikia **kilo 960** kwa siku, kwa kiwango cha juu kabisa cha kimataifa (***999.9 purity***). Na hii ni changamoto kwa Serikali na Wachimbaji kuhakikisha Kiwanda hiki na vingine vilivyojengwa vinapata malighafi.

- Manufaa ya Mtambo huu pia tumeyasikia. *Kwanza*, kuongeza mapato ya Serikali kupitia mrabaha, tozo za

ukaguzi na ushuru wa huduma; *pili*, utatoa ajira za moja kwa moja **120** na zisizo za moja kwa moja **400**; *tatu*, utawezesha utunzaji wa tofali za dhahabu kwa wazalishaji wa ndani na nje; *nne*, utawezesha madini mengine ambata (*by products*) kuainishwa na kuthaminiwa hapa nchini; *tano,* utawezesha Benki yetu Kuu kuanza kununua dhahabu na kuwezesha nchi yetu kuwa na amana ya dhahabu (yaani *Gold Reserve*).

- Sambamba na hilo, Mradi huu utasaidia kuchochea shughuli za uchimbaji madini kwenye Ukanda wa Ziwa, ambako takriban **asilimia 90** ya dhahabu inazalishwa kwa sasa. Vilevile, Mradi huu utakuwa chachu ya kukuza uchumi kwenye Jiji la Mwanza. Kama tulivyosikia, mbali ya kujenga Mtambo huu, Wawekezaji wametenga mtaji wa takriban **Dola za**

**Marekani milioni 154.5** sawa na **shilingi bilioni 346.5** kwa ajili ya kununua dhahabu.

- Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wawekezaji kwa kujenga Mtambo huu. Kama tulivyosikia, Mradi huu una wabia watatu: STAMICO, kwa niaba ya Serikali; Kampuni ya Falme ya Kiarabu ya *Rozella General Tradig LLC* pamoja na Kampuni ya *ACME Consultant Engineers PTE Ltd* kutoka Singapore. Na kwa mujibu wa Mkataba, hisa za STAMICO zitakuwa zikiongezeka kadri miaka inavyoendelea.

**Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;**

- Ni ukweli usiopingika kuwa, tangu Serikali imefanya Mabadiliko ya Sheria ya Mwaka 2017, licha ya

changamoto chache zilizojitokeza, mafanikio makubwa yamepatikana kwenye sekta ya madini. Miongoni mwa mafanikio hayo, ni kuongezeka kwa mapato ya madini kutoka **shilingi bilioni 168** mwaka 2015/2016 hadi **shilingi bilioni 528** mwaka 2019/2020; ambapo kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia tarehe 6 Juni, 2021 zilikuwa zimekusanywa **shilingi bilioni 544.585**; ambapo lengo la mwaka lilikuwa **shilingi bilioni 526**.

- Mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa masoko **39** na vituo **50** vya kuuzia madini; kutolewa kwa leseni nne za usafishaji (refinery) kwa madini ya dhahabu (Dodoma, Mwanza na Geita) na leseni 4 nyingine za ujenzi wa Mtambo wa Uyeyushaji (*Smelter*) pamoja na leseni moja ya Uchimbaji mkubwa wa Madini ya

Dhahabu Nyanzaga uliopo Sengerema kwenye Mkoa huu wa Mwanza.

- Kutokana na mafanikio hayo, mchango wa sekta ya madini umeogezeka kutoka **asilimia 4.4** mwaka 2017 hadi kufikia **asilimia 6.**7 mwaka 2020. Hii inatupa matumaini kuwa azma yetu ya kuifanya sekta ya madini kuchangia **asilimia 10** ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2025 itaweza kutimia. Napenda kutumia fursa hii, kumshukuru, ingawa hatupo naye, Hayati Rais wetu wa Awamu ya Tano, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kusimamia mageuzi haya. Naupongeza pia Uongozi wa Wizara ya Madini pamoja na wadau wote wa madini nchini, wakiwemo wachimbaji wetu wadogo, kwa kuwezesha kupatikana kwa mafanikio

haya. Bila wachimbaji, mafanikio haya yasingepatikana.

**Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;**

- Kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kutoa wito kwa Wizara kuendelea kuimarisha usimamizi wa sekta hii, ikiwemo kudhibiti wizi/utoroshaji na biashara ya magendo ya madini. Na mojawapo ya maeneo mnayotakiwa kuimarisha usimamizi ni katika Mgodi wetu Tanzanite wa Mirerani. Kama mnavyofahamu, madini haya yanapatikana hapa Tanzania pekee. Hivyo, ni wajibu wetu kukuhakiksha tunayasimamia vizuri ili yatunufaishe na kuitangaza nchi yetu. Na katika hilo, kwa mtazamo wangu, njia mojawapo ya kuweza kufanikisha hilo, ni kuanzisha Kampuni au

Taasisi itakayosimamia madini haya kuanzia kwenye uchimbaji, ununuzi na uuzaji wake. Naamini, kwa kufanya hivyo, tutaweza kudhibiti wizi na biashara holela ya madini haya. Hivyo basi, natoa rai kwako Mheshimiwa Waziri kukutana na wadau ili muweze kulitafakari suala hili.

- Sambamba na hilo, naihimiza Wizara ya Madini kuendelea kutenga maeneo kwa wachimbaji wetu wadogo. Uzoefu tulioupata kwenye miaka hii michache unaonesha kuwa, wachimbaji wadogo wakiwezeshwa kwa vifaa, mataji na mafunzo wanatoa mchago mkubwa sana. Hivyo, hamna budi kuendelea kuwatengea maeneo na kuwajengea uwezo. Na hapa, niwatake Wizara kufuatilia watu waliochukua maeneo bila ya kuyaendeleza ili kama hawana uwezo wa

kuyaendeleza, tuwanyang'anye na kuwapatia wawekezaji wengine watakaoweza kuyaendeleza na hivyo kuchangia ukuzaji uchumi wa nchi yetu.

- Na katika hilo, nitumie fursa hii pia kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye sekta ya madini. Nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa madini, ikiwemo dhahabu, shaba, almasi, madini ya fedha, chuma, makaa ya mawe pamoja na vito vya thamani. Hata hivyo, hapa nina jambo ningependa kulisema kuhusu uchimbaji madini ya chuma kule Liganga na Mchuchuma. Kama mnavyofahamu, suala hili limekuwepo kwa muda mrefu. Mwaka 2015, Serikali ilisaini Mkataba na mwekezaji lakini mpaka sasa uchimbaji haujafanyika kutokana na urasimu kwa upande wa Serikalini na pia matatizo binafsi ya

mwekezaji. Siku chache zilizopita, nilikutana na Mwekezaji huyo nikiwa na baadhi ya Watendaji Kimsingi, Serikali tumekubaliana kushughulikia changamoto zilizokuwepo. Kwa hiyo, hivi sasa tunampa muda Mwekezaji huo, lakini tukiona anasuasua, hatutasita kuachana naye na kumtafuta mwekezaji mwingine. Lengo la Serikali ni kutaka kuona chuma hicho kinachimbwa ili kiweze kutumika hapa nchini na kuuzwa nje ya nchi.

- Napenda pia kutumia fursa hii kuiagiza Wizara ya Madini kuendelea kukiimarisha Kituo cha Jemolojia Tanzania (*Tanzania Gemmological Centre* – TGC) kilichopo Arusha ambacho kinatoa mafunzo ya ngazi ya cheti na diploma katika fani ya teknolojia ya madini na usonara, utambuzi wa madini ya vito, ukataji na

ung'arishaji pamoja na utengenezaji wa mapambo na urembo. Chuo hiki ni muhimu sana. Kama mnavyofahamu, hivi sasa Serikali ipo kwenye mkakati wa kuimarisha vyuo vya ufundi ili kuwapa ujuzi vijana wetu kwenye fani mbalimbali. Chuo hiki kitatusaidia kuwapatia vijana wetu ujuzi wa uongezaji thamani wa madini yetu na hivyo kutimiza dhamira ya Serikali ya kutaka kuona madini yanachimbwa, yanachenjuliwa, yanasafishwa, kuyeyushwa na kutengenezwa bidhaa hapa hapa nchini. Ndiyo maana naihimiza sana Wizara kukiimarisha Chuo hiki; na endapo kuna changamoto yoyote, mtuambie ili tuweze kuzitatua kwa pamoja.

- Suala la mwisho kabisa, lakini sio kwa umuhimu, Mheshimiwa katika maelezo yake ametaja changamoto zinazokwamisha ustawi wa sekta ya madini nchini,

ikiwemo Kodi ya Ongezeko ya Thamani (VAT) kwa wachimbaji wakubwa, wa Kati na Wafanyabiashara wakati wa kuuza dhahabu yao viwandani; pamoja na VAT na Kodi ya Forodha ya **asilimia 25** kwa dhahabu inayoingizwa kutoka nje. Hii ina maana kuwa mtu akitaka kuleta dhahabu hapa nchini analazimika kulipa kodi hizo zote. Hali hii inawafanya wafanyabiashara wa nje washindwe kuleta dhahabu yao hapa nchini. Najua masuala haya ni ya Kisera na Kisheria; hata hivyo, ni kweli kuwa tunahitaji kuyatazama vizuri ili yasiwe kikwazo katika kuvutia watu kutoka nje kuleta madini yao hapa nchini.

- Baada ya kusema hayo.

***Mungu Ubariki Mtambo huu!***

*Mungu Ibariki Tanzania!*

**Nawasalimu tena kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**"Asanteni Sana kwa kunisikiliza"**